
34

# KIONGOZI CHA MWENYE KUHIJI NA MWENYE KUFANYA UMRA NA KUUZURU MSIKITI WA MTUME (S.A.W)




KIMECHAPISHWA NAKUGAWANYWA NA
OFISI KUU YA IDARA ZA MATEFUMUO YA
KIILIMU NA KUTOWA FATWA NA
KULINGANIA NA KUONGOZA
RIYADH SAUDI ARABIA

SI CHAKUUZWA

1403 H. — 1983

34

# KIONGOZI CHA MWENYE KUHIJI NA MWENYE KUFANYA UMRA NA KUUZURU MSIKITI WA MTUME (S.A.W)



KIMECHAPISHWA NAKUGAWANYWA NA OFISI KUU YA IDARA ZA MATEFUMUO YA KIILIMU NA KUTOWA FATWA NA KULINGANIA NA KUONGOZA RIYADH SAUDI ARABIA

SI CHAKUUZWA

1403 H. — 1983

# دليل الحاج والمعتمر

بالـلغــة الســواحليـة

## KITANGULIZI.

Enyi mahujaji watukufu, assalamu alaikum warahmatullahi wabarakatuhu. karibuni katika miji mitakatifu na viwanda twahara hali yakuwa muwageni wa Mwenyeezimungu. Kikundi cha kuufahamisha uislam katika hija kina furaha kuwatolea kiongozi kifupi kilicho kusanya mambo muhimu yanayo pasa kujulikana na mwenye kuhiji katika ibada yake ya hija na umra, tukianza na baadhi za nyasiya zilizo muhimu tunazojuisia wenyewe kwanza, nakuwausia nyinyi kutokana na neno la Mwenyeezimungu katika kuwasifu waja wake walo okoka na kufaulu duniani na akhera kwa kusema: —

وَتَوَاصَوْا بِالْحَقِّ وَتَوَاصَوْا بِالصَّبْرِ

"Wakausiana kushikamana na haki na

wakausiana kusubiri", na vilevile kulitumia neno lake Mwenyeezimungu: —

وَتَعَاوَنُوا عَلَى الْبِرِّ وَالتَّقْوَى وَلَا تَعَاوَنُوا عَلَى الْإِثْمِ وَالْعُدْوَانِ

"Saidianeni kufanya ya wema na kumuogopa mungu wala msisaidiane kufanya dhambi na kufanya uadui". Tunalo kutarajia bwana mwenye kuhiji niufanye umuhimu kukisoma kitabu hiki kabla ya kufanya amali yako ya Hijja upate kutimiza kwa ujuzi faradhi hii. Na utapata katika kitabu hiki yatakayo kukutosha usitake kuuliza mengi. Tunatumai ukihifadhi kitabu hiki kwa minajili ya mwaka wako huu na utakao kuja ikiwa umejaaliwa kuhiji. Kama tunavyo kuomba uwatunukie zawadi ndugu zako unaowaona wanahamu ya kukisoma ili faida ipate kuenea na ya-

patikane manufaa akipenda mungu Twawaombea nyote mungu awape hija njema na amali nzuri yenye kukubaliwa. Wassalam alaikum warahmatullahi wabarakatuhu.

Abdul-Aziz Bin Abdallah Bin Baz.
Mkurugenzi mkuu wa idarà za matefumuo ya kiilimu na kutowa fatwa na kulingania dini na kuongoza.

# NYASIYA MUHIMU

Mahujaji watukufu tunamshukuru Mwenyeezimungu kwa kuwaafikia kuhiji nyumba yake nakuizuru haram yake tunamuomba atutakabalie sisi na nyinyi amali njema na atuzidishie sisi na nyinyi thawabu. Tunawaletea nyasia hizi tukitaraji Mwenyeezimungu azijalie hija zetu sote ziwe njema na kusa'yi kwetu kuwe ni kwenye kushukuriwa.

1. Kumbukeni kuwa m'ko katika safari yenye kubarikiwa na kwenye kuhama kwenda kwa Mwenye-ezi-mungu safari iliyo simama juu ya kumpwekesha mungu na kumtakasia ibada na kuitika mwito wake na kumtwii wala hakuna lenye malipo makubwa kuliko hilo, kwani hija njeme malipo yake ni pepo.

2. Tahadharini na Shetwani asitie ugomvi katiyenu kwani yeye ni adui

anae watafutia ndia. Pendaneni kwa-ajili ya Mwenyeezimungu. Epukeni mijadala ya kumuasi Mwenyeezimun-gu, namjue kuwa mtume Muhammad (S.A.W.) Amesema:—

"Haamini mmoja wenu mpaka ampen-delee ndugu yake analojipendelea mwen-yewe"

3. Waulizeni wanaojuwa yaliyo watatiza katika mambo ya dini yenu na hija yenu. Mpaka muwe na ujuzi, mue-pukane na matatizo yenu. Mwenyeezi mungu amesema:—

Ulizeni wanaojuwa mkiwa hamjui na mtume (S.A.W.) Amesema:—

Yeyote atakae mpendelea, yeye Mwenye ezimungu, kheri atamfahamisha dini.

4. Juweni kuwa Mwenyeezimungu

ametuwekea faradhi na sunna, wala hakubali sunna kwa aliyezipoteza faradhi na mara nyingi hughafilika baadhi ya mahujajii nahakika hii, wakawaudhi waisilamu waume na wnawake ili wapate kubusu hajar-alaswad au kwenda mbio wakati wa tawafu au kwasababu ya kuswali nyuma ya maqamu au kunywa maji ya zamzam, kwa mfano na yote hayo ni sunna, ama kuudhi waislamu ni haramu. Basi vipi kufanya la haramu upate kufanya la sunna? Epukeni kuudhiana. Mwenyeezimungu atawapa thawabu na malipo makubwa.

A. Na tunawafafanulia zaidi kwa kuwaambia: Haifai kuswali jirani ya mwanamke au nyuma yake katika haramu ya Makka au mahala pengine kwa sababu yoyote, pamoja na kuwezekana

kuepuka hilo. Na yafaa kwa wanawake kuswali nyuma ya wnaume.

B. Milango ya haramu na mangilio yake ni ndia haifai kuifunga kwa kuswali mahala hapo japo kwa kuikimbilia jamaa.

C. Haifai kupinga T'awafu kwa kukaa pambizoni mwa Al-Kaaba au kuswali karibu na Al-Kaaba au kusimama karibu na Hijri Ismail au Maqam Ibrahim haswa wakati wa msongamano kwani hayo yanadhuru na kuudhi.

D. Kulibusu Hajaril-Aswad ni sunna na kuhifadhi hishma ya muislamu ni faradhi. Usipoteze faradhi kwa kusimamisha sunna. Yakutosha wakati wamsongamano kulishiria na kupiga takbiri na kuendelea na kutufu wala usipasue

safu bali fuatana nazo mpaka utoke mzunguko kwa upole.

E. Si sunna kuibusu Rukni Yamani bali huekwa mkono wakulia ikiwa hakuna msongamano na atasema wakati wakuipa mkono:

بِسْمِ اللهِ وَاللهُ أَكْبَرُ

BISMILLAHI WALLAHU AKBAR

na mwisho tunawausia watu wote wajilazimishe kushikamana na Qu'rani na Sunna (Ya Mtume S.A.W.)

Mtwiini MwenyeeziM'ngo na Mtume wake ili mpate kurehemewa

## YENYE KUHARIBU UISLAMU

Ndugu muislamu yataka ujue kuwa kuna mabmo yenye kuuharibu Uislamu na yanayo patikana kwa wingi, ni mambo kumi; basi kuwa na hadhari nayo:—

LA KWANZA:

Ni kushirikisha katika kuabudu. Mwenyeezimungu amesema: Hakika mwenye kumshirikisha Mwenyeezi mungu, mngu amemuharamishia pepo na mahala pake ni motoni wala madhalimu hawana yeyote wakuwanusuru. Nanikatika kushirikisha Mwenyeezi mungu kuwaomba walokufa na kutaka kuokolewa nawao na kuwaekea nadhiri na kutinda kwa ajili yao.

PILI :

NA NI KATIKA HAYO :

a Kuitakidi kwamba mipango na kanuni zilizo wekwa na watu ni bora kuliko sheria ya kiislamu, au mpango wakiislamu hausilihi kufuatwa katika karne ya ishirini. Au kuwa uislamu ndio sababu ya kuweko nyuma waislamu au uislamu unahusu mafungamano ya mtu na m'ngu wake haungilii mambo mengine ya maisha.

TATU :

Kusema kwamba kupitisha hukmu ya m'ngu kwa kukata mkono wa alie iba au kupigwa mawe muhswan alie zini hayatukuani hayo na wakati wa kisasa.

LA N'NE:

Kuitatidi kwamba yafaa kuhukumu kwa hukmu isio kuteremshwa na Mwenyeezimungu katika matangamano ya kisharia au ahadi au mambo mengine japo asiitakidi kuwa hilo ni bora kuliko hukmu ya sharia sababu kuitakidi hivyo itakuwa amehalalisha lilo haramishwa na Mwenye M'ngu kwa kuafikiana wanavyoni wote, na kila alilo haramisha Mwenyeezi M'ngu linalo julikana katika dini, kama kuzini, mvinyo, ribaa, kuhukumu kwa isio kuwa sharia ya Mwenyeezimungu. Mtu huyu atakuwa kafiri kwa kuafikiana waislamu wote.

LA TANO :

Mwenye kutukia kitu alicho kuja nacho mtume ( S.A.W. ) kuwa ni sharia, japo akakifanya, itakuwa amekufuru kwa

ushuhuda wa neno lake Mwenyeezi mungu alipo sema :

«ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ كَرِهُوا مَا أَنزَلَ اللَّهُ فَأَحْبَطَ أَعْمَالَهُمْ»

(Hilo nikwamba wao wametukia lilo teremshwa na Mwenyeezimungu akazibatilisha amali zao)

LASITA :

Mwenye kukifanyia maskhara kitu chochote katika dini ya mtume ( S.A.W. ) au thawabu zake au adhabu atakua kafiri kwa ushuhuda wa neno lake Mwenyeezi M'ngu :

قُلْ أَبِاللَّهِ وَآيَاتِهِ وَرَسُولِهِ كُنتُمْ تَسْتَهْزِئُونَ لَا تَعْتَذِرُوا قَدْ كَفَرْتُم بَعْدَ إِيمَانِكُمْ

,,SemaE Muhammad! mnamfanyia maskhara, M'ngu na aya zake na mtume wake musitoe udhuru mumekufuru baada ya kuamini kwenu"

LASABA :

Uganga na ni katika uganga unaojulikana kwa kutenga. Maana yake kumtenga mtu asimpende mkewe na amtukie na ni katika uganga kumpendezesha mwanadamu asicho kipenda kwa ndiya za kishetwani.

Mwenye kulifanya hilo au akaliridhia, huwa kafiri kwa ushuhuda wa neno lake Mwenyeezimungu :

وَمَا يُعَلِّمَانِ مِنْ أَحَدٍ حَتَّىٰ يَقُولَا إِنَّمَا نَحْنُ فِتْنَةٌ فَلَا تَكْفُرْ

Wala hawamfundishi yeyote mpaka wamwambie hakika sisi ni mtihani basi usikufuru.

LANANE :

Kuwatilia nguyu wenye kumshirikisha

Mwenyeezimungu na kuwapa misaada kinyume cha waislamu kwa dalili ya neno la Mwenyeezi M'ngu :

وَمَن يَتَوَلَّهُم مِّنكُمْ فَإِنَّهُ مِنْهُمْ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ

"Na yoyote atakae kuwafanya wao ni marafiki atakuwa ni katika wao hakika Mwenyeezimungu hawaongozi madhalimu"

LATISA :

Mwenye kuitakidi kwamba baadhi ya watu wanaweza kuepuka sharia ya mtume Muhammad (S.A.W.) huyu atakuwa kafiri kwa dalili ya neno la Mwenyeeezimungu :

وَمَن يَبْتَغِ غَيْرَ الْإِسْلَامِ دِينًا فَلَن يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِي الْآخِرَةِ مِنَ الْخَاسِرِينَ

Na anaetaka dini isio kuwa ya kiislamu hatokubaliwa nae akhera atakuwa katika wenye kukhasirika ,,

LA KUMI :
Kuipa mgongo kabisa dini ya Mwenye ezimungu au ambacho uis-lamu hauwezi kuwa sawa illa kwa kituhicho asijifunze wala asikitumie kwa dalili ya neno la Mwenyeezimungu :

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّن ذُكِّرَ بِآيَاتِ رَبِّهِ ثُمَّ أَعْرَضَ عَنْهَا إِنَّا مِنَ الْمُجْرِمِينَ مُنتَقِمُونَ

(Hakuna alie dhalimu kushinda alie kumbushwa aya za Mwenyeezimungu kisha akazipa mgongo hakika sisi ni wenye kuwatesa walio waovu)
Na amesema Mwenyeezimungu :

وَالَّذِينَ كَفَرُوا عَمَّا أُنذِرُوا مُعْرِضُونَ

"Walio kufuru ni wenye kuyapa mgongo

walio khofishwa nayo"

Hakuna tafauti baina ya zenye kuyatangua uislamu zote, kwa aliesema kwa mzaha au kikweli na Mwenye kuogopa illa Menwe kulazimishwa kwa ngugu.

Twajilinda kwa Mwenyeezimungu na mambo yenye kutuletea adhabu zake na mateso yake makali.

# NAMNA YA KUTEKELEZA IBADA YAKO YA HIJJA NA UMRAH NA KUZURU MSIKITI WA MTUME (S.A.W.)

Ewe muislamu mtukufu :

Kuna sampuli tatu za kuyafanya hayo :

1. Tamattui
2. Qirani
3. Na-Ifradi

1. Tamattui: Ni kuhirimia umrah katika miezi ya hijja (mfungo mosi, mfungo pili na siku kumi za mfungo tatu) akisha maliza umrah ahirimie hijja makkah au karibu ya makkah siku ya tarehe nane mwaka wa umrah yake hiyo.

2. Qirani: Nikuhirimia umrah na hijja pamoja, wala hazifungui mwenye kuhijji mpaka siku ya kutinda au ahirimie umrah kisha aitie hijja ndani ya umrah kabla yakuanza kutufu tawafu ya umrah.

3. Al-Ifradi: Nikuhirimia hijja kwenye miqati au makkah ikiwa ndipo anapo ishi au mahala pengine popote pakiwa pako ndani ya miqati - (mahala pa kuhirimia) kisha atabaki na ihramu yake mpaka siku ya kutinda ikiwa anae mnyama, ikiwa hana mnyama itakuwa sharia kwake nikuibadilisha hijja yake aifanye umrah atufu naasa'yi na apunguze nywele kisha afungue ihramu yake kama alivyo amrisha mtume (S.A.W.) walo hirimia hijja wakawa hawana wanyama na hivihivi atafanya aliye hijji

hijja qirani ikiwa hana mnyama itafaa kubadilisha qirani yake kwa tuliyo tangulia kuyataja, na ibada bora katika namna tatu, ni tamattui kwa asiyekuwa na mnyama sababu m'ume (S.A.W.) aliwaamrisha maswahaba wake na akawasongeza kufanya hivyo.

## NAMNA YA KUFANYA UMRAH :

1. Ukifika Miqat (Mahala Pakuhirimia) oga na ujitie manukato ikiwezekana kisha uvae nguo za kuhirimia kitambi na shuka na nivyema ziwe nycupe, mwanamkk atavaa nguo anayotaka bila kujitolea wazi kwa mapambo kisha utanuia kuhirimia umrah na Utasema :

(Ewe mola mimi nime nuia umrah nisahilishia na unikubalie)

Wanaume watajihirisha Talbiyah wala hawatajihirisha wanawake. Na utaleta kwa wingi talbiyah na kumtaja Mwenyeezimungu na Kuomba maghfira na **kuamrisha mema na kukataza mabaya.**

2. **Ukifika Makkah zunguka Al-kaaba mara saba, utaanzia Hajar Aswad na huku ukileta Takbira na utakomea hapo hapo ulipo anzia, utamtaja** Mwenyeezimungu na utaomba utakalo, dhikri au dua, kisha utaswali **nyuma ya Maqam Ibrahim ingawa mbali napo ikiwezekana. Ikitowezekana,** basi utaswali popote.
3. **Kisha toka wende Swafaa upande juu ukielekea Al-Kaaba umhimidi Mwen-** M'ngu na upige Takbira tatu hali yakuinua mikono ukariri Duwa mara tatu hii ndio sunna na Useme:

لَاإِلٰهَ إِلاَّ اللّٰهُ وَحْدَهُ

LAILAHA ILLALLAHU WAHDAHU

Na ukifanya upungufu wahizo hapana ubaya. Kisha teremka kwenye Swafaa Usa'yi kwa ajili ya Umrah mara saba utakwenda haraka katika Kusa'yi kwako kati ya alama mbili zenye rangi ya kijani kibiti na utakwenda mwendo wako wa kawaida kabla ya kuzifikia alama hizo na baada ya kuzipita kisha utapanda Marwah. Utamuhimidi Mwenyeezi M'ngu na ufanye kama ulivyo fanya ulipokuapo juu ya swafaa naupige takbiri ukiweza. Wala haina tawafu na Sa'yi Dua fulani ilo husiwa bali mwenye kutufu na mwenye Kusa'yi ataleta Dhikri na Dua awezayo au atasoma Qur'ani.

4. Ukisha timiza Kusa'yi kwako utanyoa au utapunguza nywele zako za kitwani. Hivyo huwa imetimu Umrah yako na baadaye itakuwa ni halali kwako kila lilokatazwa kwa sababu ya Ihram! Ikiwa hija yako ilikuwa ni ya Tamattui itakulazimu utinde mnyama siku ya kutindwa. Mbuzi mmoja tuu, ngamia au n'gombe kwa kushirikiana watu saba. Usipopata mnyama wa kumtinda itakulazimu kufunga siku kumi.

## NAMNA YA AMALI YA HIJJA

1. Ikiwi utahiji Ifradi au Qirani (hijja **na umrah pamoja) utahirimia kwenye miqati utakayo ifikia. Ikiwa uko duni ya miqati utahirimia ulilo linuia pale mahala ulipo, ukiwa** utahiji tamattui, hirimia hijja ma-

hala ulipo siku ya tarwiya nayo ni siku ya tarehe nane mwezi wa mfungo tatu ujitie manukato ikiwezekana kisha useme labbayka hajjan labbayka Allahumma labbayka. Mpaka mwisho wake.

2. Kisha toka wende ıinaa uswali adhuhuri na al-asri, na magharib na ishaa, na al-fajri swala za rak'ah nne utaswali rak'ah mbili qasra kila swala utaswali kwa waqti wake bila ya kukusanya.

3. Jua likitoka siku ya tarehe tisa mfungo tatu utakwenda arafat kwa utulivu na uwe na hadhari na kuwaudhi mahujaji wenzako. Utaswali hapo adhuhuri na al-asri kwa kukusanya adhuhuri na al-asri pamoja, katika wakati wa adhuhuri

na utapunguza, adhani moja na kukimu mara mbili. Kisha hakikisha kuwa umeingia mipaka ya arafat na uzidishe kumtaja M'ngu na kumuomba hali ume-elekea qibla na umeinua mikono yako miwili kwa kufuata alivyo fanya mtume (S.A.W.). Arafat nzima ni mahala pakusimama utabaki ndani ya arafat mpaka jua litwe.

4. Jua likitwa utakwenda mpaka muzdalifah kwa upole na utulivu hali ya kuleta talbiyah wala usiwaudhi nduguzo waislamu. Utaswali muzdalifah, maghribi, ishaa kwa kutanguliza pamoja na kupunguza, wakati utakapofika muzdalifah kisha utabaki muzdalifah mpaka uswali al-fajri na kupambazuke asu

buhi. Utakithirisha dua na dhikri, baada ya kwisha kuswali al-fajri hali ya kuelekea qibla ukiwa umeinua mikono yako miwili kufuata vile alivyo fanya mtume (S.A.W.).

5. Kisha utakwenda minaa kabla yakutoka jua na huku ukileta talbiyah. Ikiwa utakuwa na udhuru kama wanawake na madhaifu wasio jiweza hapana ubaya kwenda minaa wakti wa nusu ya mwisho ya usiku utatukuwa vijiwe saba tu vya kuatilia kikuta cha al-aqabah ama vijiwe vilo baki utaviokota minaa.

6. Ukifika minaa fanya yafuatayo:—

a. Atilia kikuta cha al-aqabah na ukitoka karibu na makkah uta-

atilia vijiwe saba vyenye kufuatana utaleta takbiri kwa kila kijiwe.

b. Tinda mnyama ukiwa umelazimiwa na mnyama sehemu utakula mwenyewe, na sehemu utawapa mafukara.

c. Nyoa au punguza nywele zako za kitwa na kunyoa ndilo bora mwanamke atapunguza nywele kiasi cha inchi moja na kuyafanya hayo kwa mpango huu ni bora na ukitanguliza baadhi yake hapana ubaya. Ukisha kuwatilia vijiwe na ukanyoa itakuwa umefungua fungo la kwanza baada yake utavaa nguo zako naitakuwa halali kufanya uliokatazwa isipo kuwa kumuingilia mkeo.

7. Kisha utateremka kwenda makkah utatufu tawafu ya nguzo baada yake

utasa'yi ikiwa hijja yako ni ya tamattui au ukiwa hukusa'yi pamoja na tawafu ya qudumi ikiwa hijja yako ni qirani au ni ifradi. Kwa hivi itakuwa ni halali kwako kumwingilia mkeo. Yafaa kuahirisha tawafu ya nguzo mpaka baada ya siku za minaa na kuteremka makkah baada ya kuatilia vijiwe.

8. Ukisha tufu tawafu ya nguzo siku ya kutinda utaregea minaa na ulale huko usiku wa kumi namoja na kumi na mbili, na kumi na tatu-siku tatu za tashriq ukilala siku mbili inafaa.

9. Utaatilia vikuta vitatu katika siku ya pili au ya tatu utakao baki minaa baada ya kupinduka jua utaanza cha kwanza kilicho mbali

na makkah kisha cha kati kish cha Jamratulaqabah kila kimoja kwa vijiwe saba vyenye kufuatana. Utapiga takbiri kwa killa kijiwe. Ikiwa utafupisha kwa kubaki minaa kabla ya kutwa jua la siku ya pili, jua likikutwea minaa utabaki na siku ya tatu utaatilia vijiwe vile vile na lilo bora usiku wa tatu. Yafaa kwa mgonjwa na asie jiweza amueke badali yake wa kuatilia vijiwe na inafaa alofanywa naibu kwanza aatilie vijiwe vyake kisha aatilie vijiwe vya aliye mfanya naibu.

10. Ukitaka kurudi kwenu baada ya kumaliza amali za hija utatufu alkaaba tawafu widaa (yakuaga) wala haisamehewi tawafu hii asiye kuwa mwana mke mwenye hedhi au nifasi.

## YENYE KUMPASA MWENYE IHRAMU

Yanampasa mwenye ihramu ya hijja na ya umrah yanayo fuata :

1. Ajilazimisheyaliyo lazimishwa na Mwenyeezi M'ngu juu yake katika lazima za dini yake kama swala kwa nyakati zake na kwa jamaa.
2. Ayaepuke alio katazwa na Mwenye ezi M'ngu, mambo ya upuzi, ufasiqi kujadiliana na maasia.
3. Kuwata kuwaudhi waislamu kwa maneno au vitendo.
4. Kuepuka makatazo ya ihram nayo :
   a. Asikate nywele zake au chochote

**katika makucha yake na kikitoka kitu katika hivyo bila kukusu**dia hatolazimiwa na kitu chochote wakati wa ihram.

b. Asijitie manukato mwilini au nguoni au kwenye chakula chake au vinywaji vyake. Athari ya manukato ya mbeleni haina ubaya - yalobaki alojitia kabla ya kuhirimia.

c. **Asikishughulikie kiwindwa cha bara kwa kukiuwa au kwa kukifu**kuza au kusaidia juu ya hayo, **madamu ana ihramu.**

d. **Hakati Mwenye ihram na asokuwa na ihramu mti wa haramuni wala mmea wake mbichi wala haokoti kitu cha haramuni ila kwa** sababu ya kukitafutia mwenyewe

sababu mtume ameyakataza yote hayo.

e. Haposi wala hajifungii ndoa au kumfungia mwengine wala hawaingilii wanawake madamu ana ihramu wala hakumbatiani na mwanamke kwa matamaniwa. Makatazo haya ni kwa wote waume na wake.

## MAMBO YAFUATAYO YAMKHUSU MWANAMUME :

a. Hajifiniki kitwa chake kwa kitu chenye kuambatana nacho ama kujifinika kwa chandarua au sakafu ya pari au kubeba mizigo kwa kitwa hapana ubaya.

b. Havai shati na nguo zenye maana ya shati katika nguo zilizo shonwa kuzunguka mwili mzima wala kilemba wala suruali wala kofia ila ikiwa hakupata kitambaa itafaa kuvaa suruali au ikiwa hakupata viatu atavaa khofu mbili wala hapana ubaya. Na niharamu kwa mwanamke, wakati akiwa na ihramu, kuvaa soksi mbili za mikono na kusitiri uso wake kwa kitambaa cha uso au baume wa barkoa lakini akiwako mbele ya wanaume wa kando itamlazimu asitiri uso wake kwa msuani.

kama asie kuwa na ihramu.

kama asie kuwa na ihramu Mwenye ihramu akivaa nguo ya kushonwa akafinika kitwa chake, au akajitia manukato, au akakata chochote katika nywele zake, au akakata makucha yake, kwa kusahau au kwa kuto juwa hukmu yake, kwa hayo halazimiki kutowa kombozi. Naliondoe lipasalo kuondoka akumbukapo au ajuapo.

Na hufaa kuvaa viatu, na pete, na miwani, na kisikilizo cha masikio, na saa ya mkono na mshipi na ukanda ambao huhifadhiwa mali na makaratasi.

Na hufaa kubadilisha nguo, na kuzisafisha, na kuosha kitwa na muili. Na zinyanyukapo nywele pasi kukusudia, halazimiwi na chochote. Kama ambavyo halazimiwi na **chochote kwa kupatikaniwa na majaraha.**

## NAMNA YA KUUZURU MSIKITI WA MTUME (S.A.W.)

1. Ni sunna kwako kwenda madina wakati wowote kwa niya ya kuzuru msikiti wa mtume na kuswali ndani. Sababu swala katika msikiti huu ni bora kuliko swala alfu katika msikiti mwingine ila msikiti waharam ya makkah, limesemwa hilo na mtume muhammad (S.A.W.).

2. Ziyara ya msikiti wa mtume(S.A.W.) haina ihram wala talbiya wala hapana mafungamano baina ya hija na ziyara ya msikiti kabisa ukifika msikiti wa mtume (S.A.W.) utatanguliza mguu wako wa kulia wakati wa kuingia utapiga bismi-llahi

umswalie mtume na umuombe mwenye-ezi m'ngu akufungulie milango ya rehma yake na useme :

أعوذ بالله العظيم ووجهه الكريم وسلطانه القديم من الشيطان الرجيم، اللهم افتح لي أبواب رحمتك .

Vile vile imewekwa duwa hiyo wakati wa kuingia msikiti. wowote

4. Baada ya kuingia msikitini fanya haraka uswali tahiyatul-masjid na ikiwezekana kuiswali kwenye raudha itakua ni bora. Ikitowezekana utaswali popote msikitini.

5. Kisha utakwenda katika kaburi ya mtume (S.A.W.) na usimame mbele yake ikiwa umelielekea kaburi kisha

useme kwa adabu na sauti ndogo :

السَّلامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللهِ وَبَرَكَاتُهُ

Kisha umuombee rehma. Na ukisema :

اللَّهُمَّ آتِهِ الْوَسِيلَةَ وَالْفَضِيلَةَ وَابْعَثْهُ الْمَقَامَ الْمَحْمُودَ الَّذِي وَعَدْتَهُ ، اللَّهُمَّ اجْزِهِ عَنْ أُمَّتِهِ أَفْضَلَ الْجَزَاءِ

Siuovu. Kisha utazungukia kulia kidogo ili usimame mbele ya kaburi ya Abubakar (R.A.) umpisie salamu, na umuombee maghufira na rehma. Kisha utazunguka tena kidogo kulia ili usimame mbele ya kaburi ya umar (R.A.) umpisie salamu na umuombee.

6. Na ni sunna kwenda msikiti wa qubaa hali yakuwa umejitwahirisha, ili ukazuru na kuswali ndani sababu mtume (S.A.W.) alifanya hivyo na alipendezesha.

7. Na ni sunna kuzuru makaburi ya watu wa baqii na kaburi la athmani (R.A.) na mashahidi wa uhud na kaburi la hamza (R.A.) uwapisie salamu na uwaombee, sababu mtume (S.A.W.) alikua akiwazuru na akiwaombea na aliwafundisha maswahaba wakizuru makaburi waseme :

السَّلَامُ عَلَيْكُمْ أَهْلَ الدِّيَارِ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُسْلِمِينَ وَإِنَّا
إِنْ شَاءَ اللّٰهُ بِكُمْ لَاحِقُونَ نَسْأَلُ اللّٰهَ لَنَا وَلَكُمُ الْعَافِيَةَ

Hadithi Hii ipmeokewana
Muslim.

**Wala hakuna madina misikiti wala mahala popote palipo wekewa ziyara isipokuwa mahala tulizozieleza. Usiji-**

sumbue kwa kujibebesha majambo ambayo hayana thawabu bali huenda yakakuletea madhambi na Mwenyeezi m'ngu ndiye mwenye kutuafikia.

MAKOSA YANAYO FANYWA NA BAADHI YA MAHUJAJI

## KWANZA MAKOSA KATIKA KUHIRIMIA:

Mwenye kuhiji kupita miqati (mahala pa kuhirimia) ya upande wake bila kuhirimia kwenye mahala hiyo, mpaka akafika Jeddah au mahala pengine palipo ndani ya mikati ikawa atahirimia mahala hapo; kufanya hivyo ni kukhalifu maamrisho ya mtume (S.A.W.) kwamba kila mwenye kuhiji ahirimie kwenye miqati atakayo ipita.

Itamlazimu aliefanya hivyo arudie

kwenye miqati (mahala pa kuhirimia) Alipopita akahirimie ikiwezekana ikitowezekana itamlazimu atinde mnyama makkah na awape mafukara awe alikuja kwa ndia ya bara, au bahari au anga.

Akitopitia miqati yoyote katika miqati tano zinazojulikana atahirimia akielekeana na miqati ya mwanzo kuipita.

PILI: *MAKOSA KATIKA KUTUFU*:

1. Kuanza kabla ya hajar-al-aswad na wajibu ni kuanzia kwenye hajar al-aswad.

2. Kutufu ndani ya hijri ismail sababu wakati huo hawi ameizunguka al-kaba nzima. Bali huwa ni baadhi ya al-kaba, kwani hijri ni sehemu katika

al-kaba kwa hivyo tawaf yake itabatilika.

3. Kwenda dalgi nayo ni kuenda haraka kwenye mizunguko sabaa yote na hakuna dalgi ila katika mizunguko mitatu ya mwanzo katika tawafu q ıdum.

4. Kusongamana sana kwa sababu ya kubusu hajar al-aswad na mara nyingine kupigana au kutoleana matusi na hilo halifai kwa sababu ya kuudhiana na waislamu. Kutukanana haifai muislamu kumfanyia nduguyake bila haki. Kuwata kubusu haiharibu tawafu bali tawafu yake itakuwa ni swahihi japo hakulibusu na itamtosha kulishiria na kupiga takbira akilikabili japo kwa mbali.

5. Kujipangusa na hajar al-aswad kwa kutakabaraka kutokana nalo hiyo ni bid'ah isiyo msingi katika sharia, na sunna ni kulipa mkono na kulibusu tuu, ikiwezekana.

6. Kuzipa mkono pembe zote nakujipangusa kwazo. Mtume hakukipa kitu mkono katika al-kaaba isipokuwa pembe ya hajar al-aswad na rukni al-yamani.

7. Kuuhusu kila mzunguko, katika mizunguko ya tawaf, kwa duwa fulani

kwa sababu haikuthubutu kwa mtume (S.A.W.) isipokuwa kuleta takbira kila akifika hajar al-aswad na akisema kati ya hajar-al-aswad na rukni al-yamani:

رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الْآخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ

"Bwana Wetu tupe sisi duniani mazuri na akhera mazuri na utuepushie adhabu ya moto"

8. Kuinua sauti katika tawafu wanavyo fanya baadhi ya wenye kutufu au wenye kutufisha kuinua kwa namna ya kuwaletea tashwishi wenyekutufu.

9. Kusongamana kwa ajili ya kuswali kwenye maqamu ibrahim na hili ni kinyume na mwenendo wa mtume (S.A.W.) pamoja na udhia unaopatikana kwa wenye kutufu bali yamtoshea kuziswali rak'ah mbili za tawaf mahala popote msikitini.

## TATU: MAKOSA KATIKA KUSAYI:

1. Wakipanda swafaa na marwa baadhi ya mahujaji wanaishiria alkaaba kwa mikono yao wakati wa kuleta takbira kama wanavyo piga takbira wakati wa swala. Kushiria huku ni makosa, sababu mtume (S.A.W.) alikuwa akiinua mikono yake miwili mitukufu kwa kuomba akimuhimidi Mwenyeezimungu na kuleta takbira na kumuomba analo taka akiwa ameelekea kibla na ubora ni kuiletadhikri ilioletwa na mtume juu ya swafaa na marwa.

2. Kwenda haraka kwenye sa'yi baina ya swafaa na marwa katika kila mzunguko na sunna nikufanya hara-

ka kati ya alama mbili za rangi ya kijani tu na kwenda sawa kwenye mizunguko ilio baki.

## NNE: MAKOSA KWENYE ARAFAT

1. Kuteremkia baadhi ya mahujaji n'de ya mipaka ya arafat na kubaki mpaka jua kutwa kisha wakaondoka kwenda muzdalifah bila kusimama arafat haya ni makosa makubwa yanayo waharibia mahujaji hija zao. Kwa sababu hija ni arafat na wajib wa mahujaji nikuwa ndani ya mipaka ya arafat siyo n'de ya mipaka na walikusudie hilo ikitokuwa sahali kufanya hivyo wataingia arafat qabla jua kutwa, nawatabaki hapo mpaka kutwa jua na inawatosha kuingia

arafat usiku na ni usiku wakutinda wenyewe.

2. Kuondoka baadhi ya mahujaji arafat qabla ya kutwa jua na hili halifai sababu mtume (S.A.W.) alisimama arafat mpakajua likatwa kabisa.
3. Kusongamana kwa sababu ya kupanda jabal arafat na kufika kwenye kilele, haya yanaleta madhara mengi. Na arafat nzima nimahala pakusimama, kupanda jabali na vilevile kuswali kwenye jabali si sharia.

4. Kuelekea baadhi ya mahujaji jabali la arafat wakati wa kuomba na sunna ni kuelekea qibla.

5. Kusimamisha baadhi ya mahujaji vijilima vya mtanga na vijiwe siku ya arafat mahala maalum ni amáli

isiyo kuthubutu katika sharia ya m'ngu.

## TANO: *MAKOSA KATIKA MUZDALIFAH*

1. Kujishughulisha baadhi ya mahujaji mwanzo wa kuteremka kwao muzdalifa na kuokota vijiwe kabla ya dalifah na kuokota vijiwe kabla ya kidi kwamba vijiwe vya kuatilia lazi-
za muzdalifa. Na sawa ni kwamba hufaa kuokota vijiwe mahala popote katika haramu na zilo thubutu kwa mtume ni kwamba hakuamrisha kuokotwa vijiwe vya kuatilia muzdalifah na aliokotewa asubuhi wakati wa kuondoka muzdalifah baada ya kwisha kwingia minaa

na hivyo baki ya vijiwe alivitukuwa minaa. Baadhi ya mahujaji wanaosha vijiwe kwa maji na hilo sisharia.

## SITA: *MAKOSA WAKATI WA KUATILIA*:

Kuitakidi baadhi yamahujaji kwamba wanawapiga mashetwani wakati wana atilia kwa mashingo pamoja na kuwatukana mashetwani hao. Wala halikuekwa jambo la kuatilia vikuta isipo kuwa ni kwa ajili ya kusimamisha utajo wa Mwenyeezimungu.

2. Kuatilia kwao vikuta kwa Mawe makubwa au kwa viatu au kwa mbao. Huku ni kuzidisha kwenye dini ambako kumekatazwa na mtume, lilo wekwa na sharia ni kuatilia

kwanza vijiwe vidogo mfano wake, ni vijiwe vya panda vyenye kufanana na mavi ya mbuzi yasiokuwa makubwa.

3. Kusongamana kupigana kwenye vikuta vya kuatilia kwa ajili ya kuatilia lilo wekwa na sharia ni kufanya upole na kuipinda kuatilia bila ya kumuudhi yoyote, kiasi inavyo wezekana.

4. Kuatilia vijiwe vyote mara moja Kufanya hivyo huhisabiwa kimoja Namtilie kijiwe kimoja kimoja na Alete taktakbiri pamoja na killa kijiwe.

5. Kueka unaibu katika kuatilia pamoja na kuweza kwa kuogopa taabu na msongamano.

Hakufai kueka badali ila akitoweza

kuatilia mwenyewe!

6. SABAA: *MAKOSA YANAYO FANYIKA KATIKA TAWAFU YA KUAGA:*

1. Kuteremka baadhi ya mahujapi minaa siku ya kuondoka kabla ya kuatilia vikuta wakenda kutufu tawafu ya kuaga kisha wakarudi minaa wakaatilia vikuta kisha wakasafiri kuandokea minaa kuelelekea makwao itakuwa ahdi yao ya mwisho nikuatilia na mtume (S.A.W.) amesema:

'Nasiondoke yeyote mpaka iwe mwisho wa Ah'di yake ni Al-Kaaba" Tawafu ya kuaga ni lazima iwe baada ya kumaliza amali zote za Hijja na kabla ya safari kwa muda mfupi. Wala habaki tena makkah - baada yá

kutufu ila kwa kutokewa na jambo dogo.

2. Kutoka baadhi ya mahujaji msikitini baada ya kuaga kinyumenyume wakielekea Al-kaaba kwa nyuso zao wakidai kuitukuza Al-kaaba kwa kufanya hivyo. Na huu niuzushi katika Dini usiyo msingi.
3. Kuzunguka baadhi ya mahujaji kuitizama al-kaaba wakifika mlango wa msikiti mtukufu baada yakumaliza kwao tawafu yakuaga na kuomba kwao dua kama wenye kuiaga al-kaaba, nahuu ni uzuzi katika dini.

8. NANE: *MAKOSA YAPATIKANAYO WAKATI WA KUZURU MSIKITI WA MTUME (S.A.W.)*

1. Kujipangusa kwa viambaza na miti ya chuma wakati wa kuzuru kaburi

la mtume (S.A.W.). Na kufunga nyuzi na mfano wa nyuzi kwenye madirisha kwa kutaka baraka na baraka ziko katika yalio pangwa na Mwenye-ezi m'ngu na mtume wake, Na sikatika uzuzi.

2. Kwenda kwenye mapango kwenye jabali uhud. Na mfano wake pango la hiraa na pango la thaur zilizoko makkah. Na kufunga vijitambara kwenye mapango hayo na kuleta duwa zisizo ruhusiwa na mwenye-ezi m'ngu na kujipa mashida kwa kuafanya hayo yote ambayo ni uzuzi usio msingi katika sharia takatifu.

3. Kuzuru baadhi ya mahala ambazo wanazidai kuwa ni athari za mtume kama mahala alipopiga magoti ngamia na kisima cha pete au kisima cha

athman na kutukuwa mitanga mahala hizi kwa kutaka baraka.

4. Kuwaomba walio kufa wakati wa kuzuru makaburi ya baqii na makaburi ya mashahidi wa uhud. Na kutupa pesa kwenye makaburi hayo kwa kujikurubisha kwenye makaburi na kutaka baraka kwa watu wa makaburi hayo. Haya ni katika makosa makubwa, bali nishirki kubwa kama ilivyo tajwa na wenye ilmu na yakaonyeshwa kwenye Qur'ani na hadithi za mtume (S.A.W.). Sababu ibada ni ya Mwenyeezimungu peke yake. Haifai kutumia kitu chochote cha ibada kumfanyia asiekuwa Mwenyeezimungu kama duwa na kutinda na nadhiri, namfano wa hayo Mwenyeezimungu amesema;

"Hawakuamrishwa ila wamuabudu mwenye-ezi m'ngu hali yakumtakasia dini na amesema :

"Hakika misikiti ni yamwenye-ezi m'ngu usimuombe pamoja na m'ngu mtu yeyote"

Tunamuomba Mwenye ezimungu azitengeze hali za waislamu na awafahamishe wao dini na atuepushie sisi na wao fitna zenye kupoteza. Yeye ni mwenye kusikia sana nimwenye kutakabali.

## *MAONGOZI MAFUPI KWA MWENYE KUHIJI NA MWENYE KUFANYA UMRAH NA KUZURU MSIKITI WA MTUME (S.A.W.)*

Inamlazimu Mwenye Kuhiji :

1. Kufanya haraka kutubia toba ilo safi kutokana na madhambi yake yote na ajichagulie, hija yake na umrah yake, mali ya halali.

2. **Ahifadhi ulimi wake na kusema urongo kusengenya, kufitini na** kutezawatushere.

3. **Akusudie kwa hija yake na umrah** yake radhi ya Mwenyeezimungu **na nyumba ya akhera. Na ajiweke mbali na kujionyesha na kupenda kusikiwa na kutaka fakhri.**

4. **Ajifunze amali ya sharia alowekewa**

kwenye hijja yake na umrah yake na aulize yatakayo mtatiza.

5. Mwenye kuhiji akifika kwenye miqati (mahala pakuhirimia) ana khiyari baina ya hijja ya ifradi na ya tamattui na qirani.

6. Akichelea aliehirimia kutoweza ku maliza ibada yake kwa sababu ya magonjwa au kuogopa ataweka sharti kwamba nitafungua ibada yangu pale nitakapo shindwa).

7. Inaswihi hijja yamtoto mdogo, wa kiume na wakike wala haiwatoshelezei hijja yao ya faradhi.

8. Yafaa kwa mwenye ihramu kuoga na kuosha kitwa chake na kujikuna kitwa akihitajia hilo.

9. Nihalali kwa mwanamke kujiterem-

shia msuani wake kwenye uso akichelea kuonekana na waume.

10. Walilo lizoea wanawake wengi; kufunga kilemba chini ya msuani ili kuuepusha na uso, halina msingi katika sharia.

11. Yafaa kwa mwenye ihramu kufua nguo alizohirimia na baadae kuzivaa. Vile vile inafaa ku badilisha nguo nyingine.

12. Mwenye ihramu akivaa nguo ya mzunguko au akajifinika kitwa chake au akajitia manukato kwa kusahau au kutojua hatolazimika na chochote.

13. Mwenye kuhiji atakata talbiyah akifika alkaba kabla ya kuanza tawáfu ikiwa hijja yake ni tamattui au akiwa ni mwenye kufanya umrah.

14. Haikuwekwa kwenda dalgi nakujitanda machambavu ila katika tawafu ya kuegesha na kwenda dalgi inahusu mizunguko mitatu ya kwanza na inawahusu wanaume peke yao!

15. Akifanya shaka mwenye kuhijji amezunguka mizunguko mitatu au minne ataihishabu nimitatu na nihivyo hivyo akifanya shaka katika kusa'yi.

16. Hapana vibaya kuzunguka kwa nyuma ya zamzam na maqam wakati wa msongamano na msikiti mzima ni mahala pakutufu.

17. Ni katika mambo mabaya kutufu mwanamke hali ya kujipamba na kujitia manukato na kuwata kujisitiri.

18. Mwanamke akifikiwa na ada ya mwezi au nifasi baada ya kuhirimia haitofaa kutufu al-kaaba mpaka asafike.

19. Yafaa kwa mwanamke kuhirimia kwa nguo anazozitaka pamoja na kutahadhari kujifananisha na wa-ume kwa mavazi yao pamoja na kuhadhari kuonyesha mapambo ba-li wawe na mavazi yasiyo fitina.

20. Kutamka niya katika ibada nyingine isio kuwa hijja na umrah ni bid'a iliozushwa, na kujihirisha ni ubaya zaidi.

21. Ni haramu kwa mwenye kuhijji kuipita miqati (mahala pa kuhi-rimia) bila kuhirimia ikiwa ameku-sudia hijja au umrah.

22. Mwenye kuhijji na mwenye kufanya umrah wenye kuja kwa ndia ya anga watahirimia wakielekeana na miqati na sharia kwao wajitayarishe kuhirimia qabla ya kupanda ndege.

23. Mtu ambaye makao yake yako ndani ya miqati halazimishwi kwenda kwenye miqati yoyote bali pale kwenye makao yake ndiyo miqati yake ya kuhirimia hijja na umrah.

24. Wanayo fanywa baadhi ya watu kukithirisha umrah baada ya hijja kutoka tan'iim au ju'raanah hayana dalili ya kuwa ni sharia.

25. Mwenye kuhiji siku ya tarehe nane, atahirimia pale anapo kaa makkah wala hailazimu kuhirimia ndani ya makkah wala kwenye

miyzab kama wanavyo fanya watu wengi.

26. Kutoka Minaa kuelekea arafat siku ya tarehe tisa ubora ni baada ya kutoka jua.

27. Haifai kuondoka arafat qabla ya kutoka jua na ikiwa ataondoka baada ya kutwa ataondoka kwa utaratibu na upole.

28. Swala ya magharibi na isha itaswaliwa baada ya kufika muzdalifah ikiwa ni wakati wa magharibi au baada ya kuingia isha.

29. Yafaa koukota vijiwe vya kutupa mahala popote wala silazima kuziokota muzdalifah.

30. Si sunna kuosha vijiwe vya kuatilia, kufanya hivyo hakukupokewa kwa

mtume (S.A.W.) wala swahaba zake. Wala haifai kwa vijiwe vilio kwisha atiliwa.

31. Yafaa kwa wanawake madhaifu na watoto wadogo na mfano wao kwenda Minaa mwisho wa usiku.

32. Akifika mwenye kuhijji Minaa siku ya idi atakata talbiya na ataatiliya kikucha alaqaba kwa vijiwe saba vyenye kufuatana.

33. Si sharti kubakia vijiwe mahala pa kuatilia lakini ni sharti vijiwe vishukie mahala hapo.

34. Wakati wakutinda huweki mpaka kutwa jua la siku ya tatu ya siku za tashriqi kwa kauli ilio swhihi ya wanavyoni.

35. Tawafu ya nguzo au ziyara siku ya idi ni nguzo miongoni mwanguzo

za hijja, hijja haitimu mpaka ifanywe na yafaa kuicheleweesha mpaka baada ya kumalizika siku za Minaa.

36. Aliye fanya qirani hijja na umrah hana isipokuwa sa'yi moja tu vile vile mwenye kuhiji hija peke yake kisha akabaki na ihramu yake mpaka siku ya kutinda.

37. Lilobora kwa mwenye kuhiji nikupanga amali siku za kutinda ataanza kuatilia kikucha cha alakabah kisha atatinda kisha atanyao au atapunguza nywele kisha atufu alkaba kisha atasa'yi baada ya kutufu ikiwa atatanguliza au ataakhirisha litamtoshelezea.

38. Mambo ambayo huifunguwa ihramu kabisa :
   (a) Kuatilia kikuta cha Al-agabah.
   (b) Kunyowa au kupunguza.
   (c) Tawafu ya nguzo pamoja na kusa'yi.
39. Akitaka mwenye kuhiji kufanya haraka ya kuondoka Minaa itamlazimu aondoke Minaa kabla kutwa jua.
40. Mtoto mdogo asieweza kuatilia, waliyi wake ataatilia badala yake baada ya kuatilia vyake mwenyewe kwanza.
41. **Yafaa kwa asoweza kuatilia kwa sababu ya maradhi au uzee au kuwa** ni mja mzito, kumwakilisha atakaye **atilia badala yake.**
42. Yafaa kwa aliyewekwa naibu aatilie vyake kisha vya aliye mpa unaibu kila kikuta miongoni mwavikuta vitatu mahala pamoja.
43. Niwajibu kwa mwenye kuhiji

ikiwa hijja yake ni ya tamattui au ya qirani wala asiwe ni mkaazi. Waharamuni itamlazimu damu nao ni mbuzi au fungu la saba la ngamia au fungu la saba la n'gombe.

44. Mwenye hija ya tamattui au qirani akishindwa na mnyama itamlazimu afunge siku tatu huko hijja na siku saba akirudi nyumbani.

45. Ubora kwa mwenye kuhiji ni kutanguliza siku tatu qabla ya arafat ili awe siku ya arafat simwenye saumu ikito wezekana hivyo atafunga siku za tashriqi.

46. Yafaa kuzifunga siku tatu zilizotajwa kwa mfululizo, au mbalimbali.

47. Niwajibu tawafu ya kuaga kwa

killa mwenye kuhiji ila kwa mwanamke aliye fikiwa na ada ya mwezi au nifasi.

48. Ni sunna kuzuru msikiti wa mtume kabla ya hijja au baada yake.

49. Ni sunna kwa mwenye kuzuru msikiti wa mtume aanze kuswali rak'ah mbili za tahiyah mahala popote msikitini na ubora ni kuziswali kwenye rodha takatifu.

50. Kuzuru kaburi la mtume (S.A.W.) na makaburi mengine ni sharia kwa waume tu sio kwa wanawake kwa sharti asilifungie hilo safari ya kasidi !

51. Kujipangusa kwa chumba kitukufu au kukibusu au kukizunguka ni bid'a mbaya wala haikupokewa kwa wanavyoni wema walio tangu-

lia na ikiwa atakusudia kwa kuzunguka kujikurubisha kwa mtume hiyo itakuwa ni shirki kubwa !

52. Haifai kwa yoyote kumuomba mtume amkidhie haja au kumuondoshea shida hiyo ni shirki.

53. Uhayi wa mtume (S.A.W.) kaburini kwake ni uhayi wa barzakh sikama uhayi wake kabla ya kufa. Hakika huo ni uhayi haujui ulivyo wala namna yake ila Mwenyeezi mungu.

54. Wanao yafanya baadhi ya wanaozuru kukusudia kuomba kwenye kaburi la mtume (S.A.W.) hali yakuelekea kaburi na kuinua mikono nikatika bid'ah zilizo zushwa.

55. Kuzuru kaburi la mtume (S.A.W.)

siwajibu wala si sharti katika sharti za hijja kama wanavyo dhani baadhi ya watu wasiokuwa na ujuzi.

56. Hadithi zinazo shikiliwa na wanoasema nisharia kufunga safari **kwenda kaburini kwa mtume** (S.A.W.); imma sanadi zake ni **dhaifu** au **ni zakusingiziwa mtume** (S.A.W.).

# Dua Hizi Ni Vyema Kuzisoma Kwenye Arafat Na Katika Al-Mash'ar Al-Haram Na Penginepo Miongoni Mwa Mahala za Dua.

الْمُقِرُّ الْمُعْتَرِفُ إِلَيْكَ بِذَنْبِهِ أَسْأَلُكَ مَسْأَلَةَ الْمِسْكِينِ، وَأَبْتَهِلُ إِلَيْكَ اِبْتِهَالَ الْمُذْنِبِ الذَّلِيلِ، وَأَدْعُوكَ دُعَاءَ الْخَائِفِ الضَّرِيرِ، دُعَاءَ مَنْ خَضَعَتْ لَكَ رَقَبَتُهُ، وَذَلَّ لَكَ جِسْمُهُ، وَرَغِمَ لَكَ أَنْفُهُ.

وَصَلَّى اللهُ عَلَى سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِهِ وَصَحْبِهِ وَسَلَّمَ.

شَاهِدِيْ، وَتُبَيِّضُ بِهَا وَجْهِي، وَتُزَكِّي بِهَا عَمَلِي، وتُلْهِمُنِي بِهَا رُشْدِي، وَتَرُدُّ بِهَا الْفِتَنَ عَنِّي، وَتَعْصِمُنِي بِهَا مِنْ كُلِّ سُوءٍ. اللهمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ الْفَوْزَ يَوْمَ الْقَضَاءِ، وَعَيْشَ السُّعَدَاءِ، وَمَنْزِلَ الشُّهَدَاءِ، وَمُرَافَقَةَ الأَنْبِيَاءِ والنَّصْرَ عَلَى الأَعْدَاءِ. اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ صِحَّةً فِي إِيْمَانٍ، وإِيْمَانٍ فِيْ حُسْنِ خُلُقٍ، وَنَجَاحاً يَتْبَعُهُ فَلاحٌ، وَرَحْمَةً مِنْكَ وَعَافِيَةً مِنْكَ وَمَغْفِرَةً مِنْكَ وَرِضْوَاناً. اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ الصِّحَّةَ وَالْعِفَّةَ، وَحُسْنَ الْخُلُقِ، وَالرِّضَاءَ بِالْقَدَرِ. اللَّهُمَّ إنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّ نَفْسِي، وَمِنْ شَرِّ كُلِّ دابَّةٍ أَنْتَ آخِذٌ بِنَاصِيَتِهَا، إِنَّ رَبِّي عَلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ.

اللَّهُمَّ إِنَّكَ تَسْمَعُ كَلَامِي، وَتَرَى مَكَانِي وَتَعْلَمُ سِرِّي وَعَلَانِيَتِي، وَلَا يَخْفَى عَلَيْكَ شَيْءٌ مِنْ أَمْرِي وَأَنَا الْبَائِسُ الْفَقِيرُ، وَالْمُسْتَغِيثُ الْمُسْتَجِيرُ، وَالْوَجِلُ الْمُشْفِقُ

طَاعَتِكَ مَاتُبَلِّغُنَا بِهِ جَنَّتَك، وَمِنَ الْيَقِينِ مَاتُهَوِّنُ بِهِ عَلَيْنَا مَصَائِبَ الدُّنْيَا، وَمَتِّعْنَا بِأَسْمَاعِنَا وَأَبْصَارِنَا وَقُوَاتِنَا مَا أَحْيَيْتَنَا وَاجْعَلْهَا الْوَارِثَ مِنَّا، وَاجْعَلْ ثَأْرَنَا عَلَى مَنْ ظَلَمَنَا، وَانْصُرْنَا عَلَى مَنْ عَادَانَا، وَلَاتَجْعَلِ الدُّنْيَا أَكْبَرَ هَمِّنَا وَلَامَبْلَغَ عِلْمِنَا وَلاتَجْعَلْ مُصِيبَتَنَا فِي دِينِنَا وَلَا تُسَلِّطْ عَلَيْنَا بِذُنُوبِنَا مَنْ لَايَخَافُكَ وَلَايَرْحَمُنَا. اللَّهُمَّ إني أَسْأَلُكَ مُوجِبَاتِ رَحْمَتِكَ، وَعَزَائِمَ مَغْفِرَتِكَ، وَالْغَنِيمَةَ مِنْ كُلِّ بِرٍّ، وَالسَّلَامَةَ مِنْ كُلِّ شَرٍّ، وَالْفَوْزَ بِالْجَنَّةِ، وَالنَّجَاةَ مِنَ النَّارِ. اللَّهُمَّ لَا تَدَعْ لَنَا ذَنْباً إلا غَفَرْتَه، ولاعَيْباً إلا سَتَرْتَهُ، وَلَاهَمّاً إلا فَرَّجْتَهُ، وَلَادَيْناً إلَّا قَضَيْتَهُ، وَلَاحَاجَةً مِنْ حَوَائِجِ الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ هِيَ لَكَ رِضًا وَلَنَا صَلَاحٌ إلا قَضَيْتَهَا يَاأَرْحَمَ الراحمين. اللهمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ رَحْمَةً مِنْ عِنْدِكَ، تَهْدِي بِهَا قَلْبِي، وَتَجْمَعُ بِهَا أَمْرِي، وَتَلُمُّ بِهَا شَعْثِي، وَتَحْفَظُ بِهَا غَائِبِي وَتَرفع بِهَا

اللهُمَّ إني أسألك أنْ ترفعَ ذِكري، وتضعَ وِزري، وتُطهر قلبي، وتُحصنَ فرجي، وتغفرلي ذنبي، وأسألكَ الدرجاتِ العُلى مِنَ الجنَّةِ، اللهُمَّ إنّي أسألكَ أنْ تبارِكَ فيْ سَمْعِي، وفي بصري، وفي رُوحي، وفي خلقي، وفي خُلُقِي، وفي أهْلِي، وفي محيَايَ، وفي عملي، وتقبَّلْ حسناتي، وأسألكَ الدرجاتِ العُلى مِنَ الجنة.

اللهُمَّ إنّي أعوذُ بكَ مِنْ جَهْدِ البلاءِ، ودَرْكِ الشقاءِ، وسُوءِ القضاءِ، وشماتةِ الأعداءِ، اللهُمَّ مُقلِّبَ القُلوبِ، ثبِّتْ قلبيْ على دِينِكَ. اللهُمَّ مُصرِّفَ القُلوبِ والأبصارِ، صرِّفْ قلوبنا على طاعتِكَ. اللهمَّ زِدْنا ولا تنقصْنا، وأكرمنا ولا تُهنَّا، وأعطِنا ولا تحرمنا، وآثِرنا ولا تؤثِرْ علينا. اللهُمَّ أحسِنْ عاقبتنا فيْ الأمُور كُلِّها، وأجِرْنا مِنْ خِزيِ الدُّنيا وعذابِ الآخِرة. اللهمَّ اقسِمْ لنا مِنْ خشيتِكَ ماتحولُ بهِ بيننا وبينَ معصيتِكَ، ومِنْ

شُكْرَ نِعْمَتِكَ وَحُسْنَ عِبَادَتِكَ، وَأَسْأَلُكَ قَلْباً سَلِيماً، وَلِسَاناً صَادِقاً، وأَسْأَلُكَ مِنْ خَيْرِ مَاتَعْلَمُ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّ مَاتَعْلَمُ، وَأَسْتَغْفِرُكَ مِمَّا تَعْلَمُ، وَأَنْتَ عَلاَّمُ الْغُيُوبِ. اللَّهُمَّ أَلْهِمْنِي رُشْدِي، وَقِنِي شَرَّ نَفْسِي. اللَّهُمَّ إني أَسْأَلُكَ فِعْلَ الْخَيْرَاتِ وَتَرْكَ الْمُنْكَرَاتِ، وَحُبَّ الْمَسَاكِينِ، وَأَنْ تَغْفِرَ لِي وَتَرْحَمَنِي، وَإِذَا أَرَدْتَ بِعِبَادِكَ فِتْنَةً، فَتوفَّنِي إِلَيْكَ مِنْهَا غَيْرَ مَفْتُونٍ، اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ حُبَّكَ، وَحُبَّ مَنْ يُحِبُّكَ، وَحُبَّ كُلِّ عَمَلٍ يُقَرِّبُنِي إِلَى حُبِّكَ. اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ خَيْرَ الْمَسْأَلَةِ، وَخَيْرَ الدُّعَاءِ وَخَيْرَ النَّجَاحِ، وَخَيْرَ الثَّوَابِ، وَثَبِّتْنِي وَثَقِّلْ مَوَازِينِي، وَحَقِّقْ إِيمَانِي، وَارْفَعْ دَرَجَتِي، وَتَقَبَّلْ صَلاَتِي، وَاغْفِرْ خَطِيئَاتِي، وَأَسْأَلُكَ الدَّرَجَاتِ الْعُلَى مِنَ الْجَنَّةِ. اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ فَوَاتِحَ الْخَيْرِ، وَخَوَاتِمَهُ، وَجَوَامِعَهُ، وَأَوَّلَهُ وَآخِرَهُ، وَظَاهِرَهُ وَبَاطِنَهُ وَالدَّرَجَاتِ الْعُلَى مِنَ الْجَنَّةِ.

بِـكَ مِنْ أَنْ أَموتَ لَدِيغاً، وأعوذ بِكَ مِنْ طَمَعٍ يَهْدِي إلَى طَبْعٍ. اللهـمَّ إنـي أَعُوذُ بِـكَ مِنْ مُنْكَراتِ الأَخْلَاقِ وَالأَعْـمَالِ وَالأَهْـوَاءِ وَالأَدْوَاءِ، وَأَعُـوذُ بِـكَ مِنْ غَـلَبَةِ الـدَّيْنِ، وَقَهْرِ العَدُوِّ، وَشَمَاتَةِ الأَعْدَاءِ. اللهمَّ أَصْلِحْ لِي دِيـنِي، الَّذِي هُوَ عِصْمَةُ أَمْرِي، وَأَصْلِحْ لِي دُنْيَايَ التِي فِيهَا مَعَـاشِـي، وأَصْلِحْ لِي آخِرَتِي، التي إليها مَعَادِي، واجْـعَلْ الحَيَـاةَ زِيادَةً لِي فِي كُلِّ خَيْرٍ، وَاجْعَل المَوْتَ رَاحَةً لِـي مِـنْ كُـلِّ شَرٍ، رَبِّ أَعِـنِّـي وَلاَ تُـعِـنْ عَلَـيَّ، وَانْـصُرْنِـي وَلَا تَـنْصُرْ عَلَيَّ، وَاهْدِنِي وَيَسِّرْ الهُدَى لِي. اللهـمَّ اجْعَلْنِـي ذَكَّاراً لَكَ، شكَّاراً لَكَ، مِطْوَاعاً لَكَ، مُخْبِتـاً إلَـيْـكَ، أَوَّاهاً مُنِيباً، رَبِّ تَقَبَّلْ تَوْبَتِي، وَاغْسِلْ حَـوْبَتِـي، وَأَجِـبْ دَعْـوَتِي، وَثَبِّتْ حُجَّتِي، وَاهْدِ قَلْبِي وَسَدِّدْ لِسَـانِـي، وَاسْلُلْ سَخِـيمَةَ صَدْرِي. اللَّهُمَّ إني أَسْأَلكَ الثَّبَاتَ فِي الأَمْرِ، وَالعَزِيمَةَ عَلَى الرُّشْدِ، وَأَسْأَلُكَ

لَا يَصْرِفُ عَنِّي سَيِئَهَا إلا أنْتَ. اللهم أَصْلِحْ لِي دِيْنِي، وَوَسِّعْ لِي فِي دَارِي وَبَارِكْ لِي فِيْ رِزْقِي. اللهم إنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ الْقَسْوَةِ وَالْغَفْلَةِ وَالذِلَّةِ وَالْمَسْكَنَةِ وَأَعُوذُ بِكَ مِنَ الْكُفْرِ وَالْفُسُوقِ وَالشِّقَاقِ وَالسُّمْعَةِ وَالرِّ يَاءِ.

وَأَعُوذُ بِكَ مِنَ الصَّمَمِ وَالْبُكْمِ وَالجُذَامِ وَسَيِّءِ الأَسْقَامِ. اللهم آتِ نَفْسِي تَقْوَاهَا، وَزَكِّها، أَنْتَ خَيْرُ مَنْ زَكَّاها، أَنْتَ وَلِيُّهَا وَمَوْلَاهَا، اللهمَّ إِنِّي أَعُوذبكَ مِنْ عِلم لَا يَنْفعُ، وَقَلْبٍ لَا يَخْشَعُ، وَنَفْسٍ لَا تَشْبَعُ، وَدَعْوَةٍ لَا يُسْتَجَابُ لَهَا، اللَّهُمَّ، إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّ مَاعَمِلْتُ، وَمِنْ شَرِّ مَا لَمْ أَعْمَلْ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّ مَاعَلِمْتُ، وَمِنْ شَرِّ مَا لَمْ أَعْلَمْ، اللهمَّ إني أعوذُ بِكَ مِنْ زَوَالِ نِعْمَتِكَ، وَتَحَوُّلِ عَافِيَتِكَ، وَفَجَاءَةِ نِقْمَتِكَ، وَجَمِيعِ سَخَطِكَ. اللهمَّ إنِّي أعوذُ بِكَ مِنَ الْهَدْمِ والتَّرَدِّي وَمِنَ الْغرقِ وَالحرقِ والْهرم، وَأَعُوذ بكَ مِنْ أَنْ يَتَخَبَّطَنِي الشَّيْطَانُ عِنْدَ الْموتِ، وأعوذُ

بكَ مِنْ شَرِّ مَا صَنَعْتُ، أَبُوءُ لَكَ بِنِعْمَتِكَ عَلَيَّ، وَأَبُوءُ بِذَنْبِي، فَاغْفِرْ لِي، إِنَّه لايَغْفِرُ الذُّنُوبَ إِلَّا أَنْتَ. اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ الْهَمِّ وَالْحَزن، وَأَعُوذُ بِكَ مِنَ الْعَجْزِ وَالْكَسَلِ، وَمِنَ الْبُخْلِ وَالْجُبْنِ، وَأَعُوذُ بكَ مِنْ غَلَبَةِ الدَّيْنِ، وَقَهْرِ الرِّجَالِ. اللَّهُمَّ اجْعَلْ أَوَّلَ هٰذَا الْيَوْمِ صَلَاحاً وأَوْسَطَهُ فَلَاحاً، وَآخِرَهُ نَجَاحاً، وَأَسْأَلُكَ خَيْرَيِ الدُّنْيَا وَالآخِرَةِ يَاأَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ. اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ الرِّضَى بَعْدَ الْقَضَاءِ، و برد الْعَيْشِ بَعْدَ الْمَوْتِ، وَلَذَّةَ النَّظَرِ إلى وَجْهِكَ الْكَرِيمِ، وَالشَّوْقَ إِلى لِقَائِكَ، فِي غَيْرِ ضَرَّاء مُضِرَّة، وَلَافِتْنَة مُضلّة، وأَعُوذُ بكَ أَنْ أَظْلِمَ أو أُظْلَم، أَوْ أَعْتَدِيَ أَوْ يُعتَدى عَلَيَّ، أَوْ أَكْتَسِبَ خَطِيئَةً أو ذَنْباً لا تَغْفِرُهُ.. اللَّهُمَّ إِنِي أَعُوذُ بكَ أَنْ أُرَدَّ إِلى أَرْذَلِ الْعُمُرِ. اللَّهُمَّ اهْدِني لِأَحْسَنِ الأَعْمَالِ والأَخْلَاقِ لَايَهْدِي لِأَحْسَنِهَا إِلَّا أَنْتَ.. وَاصْرِف عَنِّي سَيِّئَهَا

# أدعيـــة

يُناسب الدعاء بها أو ماتيسر منها في عرفات وفي المشعر الحرام وفي غيرها من مواطن الدعاء.


اَللّٰهُمَّ إنِّي أَسْأَلُكَ الْعَفْوَ وَالْعَافِيَةَ فِي دِيْنِي وَدُنْيَايَ وَأَهْلِي وَمَالِي. اَللّٰهُمَّ اسْتُرْ عَوْرَاتِيْ، وَآمِنْ رَوْعَاتِي اَللّٰهُمَّ احْفَظْنِي مِنْ بَيْنِ يَدَيَّ وَمِنْ خَلْفِيْ، وَعَنْ يَمِيْنِي وَعَنْ شِمَالِي وَمِنْ فَوْقِي، وَأَعُوْذُ بِعَظَمَتِكَ أَنْ أُغْتَالَ مِنْ تَحْتِي.

اَللّٰهُمَّ عَافِنِي فِي بَدَنِي اَللّٰهُمَّ عَافِنِي فِيْ سَمْعِي، اَللّٰهُمَّ عَافِنِي فِي بَصَرِيْ. لَا إلٰهَ إِلَّا أَنْتَ. اَللّٰهُمَّ إِنِّي أَعُوْذُ بِكَ مِنَ الْكُفْرِ وَالْفَقْرِ وَمِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ، لا إله إلَّا أَنْتَ. اَللّٰهُمَّ أَنْتَ رَبِّي لَا إِلٰهَ إِلَّا أَنْتَ خَلَقْتَنِي، وَأَنَا عَبْدُكَ، وَأَنَا عَلَى عَهْدِكَ وَوَعْدِكَ مَا اسْتَطَعْتُ، أَعُوذُ

# دليل الحاج والمعتمر
## وزائر مسجد الرسول صلى الله عليه وسلم

٣٤

باللغة السواحلية



طبع ونشر

الرئاسة العامة لإدارات البحوث العلمية والإفتاء والدعوة والإرشاد

الرياض ـ المملكة العربية السعودية

١٤٠٣ هـ - ١٩٨٣ م